# THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
# NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL
# CERTIFICATE OF SECONDARY EDUCATION EXAMINATION

**021** **KISWAHILI**

(Kwa Watahiniwa Walioko na Wasiokuwa Shuleni)

**Muda: Saa 3** **6 Novemba 2001 asubuhi**

---

**Maelekezo**

1. Karatasi hii ina sehemu A, B, C, D na E.
2. Jibu maswali YOTE kutoka sehemu A, B, C na D na maswali MAWILI (2) kutoka sehemu E. Swali la 12 ni la lazima.
3. Zingatia maagizo ya kila sehemu na ya kila swali.
4. Andika Namba yako ya Mtihani katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

Karatasi hii ina kurasa 6 zenye maandishi



Find more free educational resources at http://maktaba.tetea.org

## SEHEMU A (Alama 10)

## UFAHAMU

1. Soma kifungu cha habari kifuatacho kisha jibu maswali kwa kuandika herufi ya jibu sahihi katika kijitabu chako cha kujibia.

Watu wote walirudi makwao. Shida ilienea katika nchi ya Kufikirika. Watu walikuwa hawakufanya kazi kwa muda wa miaka sita mfululizo kwa sababu wote walishughulika katika kutafuta tiba ya ugumba wa Mfalme na utasa wa Malkia.

Hasara zilizotokea katika muda ule zilikuwa ni kubwa na nyingi; Kubwa na nyingi hata zilikuwa hazilingani na hasara zozote nyingine ambazo watu wa Kufikirika waliweza kukumbuka kuwa waliziona zamani katika nchi yao. Mashamba yalitupwa. Mitambo, vinu na viwanda vilikuwa havina watu. Mazizi na ghala zilikuwa tupu kabisa. Nusu ya sarafu na majohari katika hazina ilipotea. Kazi katika mashimo na nyingine zilifungwa. Waandishi walitupa chini kalamu zao na wanachuoni waliacha vitabu vyao wazi.

Nchi ambayo zamani ilikuwa ya shibe, utajiri, nguo, tafrija na neema zote sasa ilikuwa imegeuka nchi ya njaa; umaskini na uhitaji wa kila namna ulikuwa mbele ya watu. Maisha haya mapya yalisumbua watu sana hata yakawa hayavumiliki. Afya ya watu ilitishwa na maradhi. Vifo vilitokea kwa wingi mno. Shida hii ilipasa kuzuiwa au Wafikirika wote wangalipanguswa katika uso wa ardhi. Ilikuwa ni wajibu wa kila mtu kutenda awezavyo kujisaidia mwenyewe, watoto wake na nchi yake. Basi baada ya marejeo kila mtu alijitia katika kazi yake tena kwa bidii zote.

Isipokuwa watoto, Wafikirika wote walikuwa wana desturi ya kufanya kazi kwa muda mwingi kuliko watu wote katika mataifa mengine ya dunia. Muda wa kufanya kazi katika nchi yao ulikuwa ni saa kumi na mbili. Saa mbili zilitumiwa kwa maburudisho katika michezo, saa mbili nyingine zilikuwa ni za mapumziko na saa nane ni za kulala katika kila saa ishirini na nne au siku moja. Vitanda vilikuwa havina watu juu baada ya muda wa saa nane za kulala isipokuwa wagonjwa na watoto wadogo tu. Kama si kwa sababu ya faida ya afya hata saa nane za kulala zingalipunguzwa kuwa saa saba au sita tu. Shauri la kupunguza wakati wa kulala lilipelekwa mbele ya madiwani wa nchi ya Kufikirika na wasimamizi wa kazi. Lilikubaliwa na halmashauri ndogo lakini halikufaulu katika halmashauri kuu kwa sababu ilidhaniwa kuwa hofu ya hatari juu ya maisha itakuwa kubwa sana. Kwa hivi halikupata idhini ya serikali. Wafikirika walikuwa na umoja madhubuti ambao ulisimama imara mbele ya machafuko yoyote. Shauri moja jema lilikubaliwa na kushangiliwa na wote na baya lilikataliwa na kila mtu.

Wafikirika waliweza kufanya kazi bora na za kuajabisha mno wakati watu wa mataifa mengine walipokuwa wamo katika usingizi, uvivu, anasa au uzembe. Kutwa walikuwa katika kazi na katika fikira za kujistawisha. Mtu ambaye hafanyi kazi kwa muda wa saa kumi na mbili alikuwa na aibu kwa wenziwe; hasara kwa serikali na kwake mwenyewe. Kumwita mtu mvivu katika Kufikirika ilikuwa si **dhihaka** ya kusameheka ila hatia kubwa mno kwa sababu nchi hiyo haikuwa na mtu mvivu hata mmoja. Kwa sheria za Kufikirika uvivu ulikuwa una tafsiri ya wizi wa wakati. Mwizi wa wakati alipatilizwa kwa adhabu ngumu sawa na mwizi wa mali au kitu kingine. Kazi kubwa, ngumu na nzito kwa watu wa Kufikirika zilikuwa ni sawasawa kabisa na mabandia ya mchezo kwa watoto wadogo. Ari ya kila mtu ilikuwa ni kutenda tendo kubwa na lililo bora kuliko mwingine. Hii ni desturi inayodumu hata sasa katika nchi ya Kufikirika.

MASWALI

(i) Kichwa cha habari kinachofaa kwa habari hii ni

A Kufikirika
B Kilimo katika nchi ya Kufikirika
C Matokeo ya kutokufanya kazi
D Maisha ni shida
E Maisha mapya yenye faraja.



Find more free educational resources at http://maktaba.tetea.org

(ii) Wananchi wa Kufikirika waliacha kufanya kazi kwa muda mrefu kwa sababu

A walikuwa wamechoka
B walipewa likizo
C mfalme wao alikuwa mgonjwa
D Malkia alikuwa mgonjwa
E walikuwa wanatafuta tiba ya Mfalme wao na mke wake.

(iii) Mwandishi anaposema "shida hii ilipasa kuzuiwa au Wafikirika wote wangalipanguswa katika uso wa ardhi" ana maana kuwa

A watalazwa ardhini
B wangekufa
C watalima mazao mengi
D watavuna mazao bora
E watawajibika ipasavyo kwa mfalme wao.

(iv) Wananchi wa Kufikirika waliipenda kazi kuliko usingizi kwa sababu

A muda wao mwingi waliutumia kufanya kazi
B ilikubaliwa na halmashauri yao
C waliamriwa hivyo na serikali yao
D waliogopa machafuko
E walikuwa tayari kupunguza muda wao wa kulala kufikia saa saba au sita kwa siku.

(v) Shauri la kuongeza saa za kufanya kazi lilipelekwa mbele ya madiwani na hawa

A walikubaliana na pendekezo hili
B walipinga muswada huo
C walikubaliana lakini wakalipeleka mbele kwa uamuzi
D walifurahia bila kutoa uamuzi
E waliwafukuza walioleta pendekezo hilo.

(vi) Mwandishi anasema usingizi unamsaidia Mwanakufikirika kuwa

A mpiganaji bora
B mfanyakazi mwenye uchovu
C mwananchi mwenye afya bora
D mnyonge
E mkulima hodari.

(vii) Mwandishi anaposema "Umoja madhubuti uliosimama imara" ana maana ya

A umoja sharti usimame
B umoja usiotetereka
C umoja si nguvu
D kupata idhini ya serikali
E umoja ni dhihaka inayosameheka.

(viii) Asiyefanya kazi katika nchi ya Kufikirika alifananishwa na

A jangili
B mvivu wa kutupwa
C mwizi wa mali au kitu chochote
D mpenda anasa
E mzembe.



Find more free educational resources at http://maktaba.tetea.org

(ix) Mwandishi anaposema "anapatilizwa" ana maana kuwa

A anafanya jambo
B anahukumiwa
C anasamehewa
D anapokewa
E anabatizwa.

(x) Juhudi ya kutokubali kushindwa bali kufanikiwa ulioneshwa na kila Mwanakufikirika kwa

A kufanya kazi kila siku
B kutumia muda wao kuburudika
C kupenda michezo
D kufanya kila jambo vizuri zaidi kuliko Mwanakufikirika mwingine
E kuwa mabandia wa michezo.

2. Soma kifungu cha habari kifuatacho kisha andika ufupisho wa maneno 40.

Siku moja jioni mfalme alikuwa nje katika bustani. Maua yaliyokuwa yamechanua yalivuta macho na harufu zake nzuri zilipendeza pua. Sauti ya ndege waliokuwa wakiimba matawini kwa kuagana na mchana ilikuwa na simanzi kidogo masikioni. Magharibi jua lilitua. Mashariki mwezi ulitokeza na hewa ilikuwa baridi. Mfalme alikuwa na mazoea ya kuona mabadiliko kama yale ya siku zote lakini siku ile hali ya mambo ilifungua mlango wa fikira ngeni katika ubongo wake. Alitazama huku na huko akawaza kuwa kama mahali pa jua hushikwa na mwezi au nyota juu ya mbingu na mahali pa joto huja baridi, lakini nani atashika mahali pake akifariki! Alirudi kwake na wingi wa mawazo lakini alikuwa na hadhari kubwa ya kuficha siri kwa malkia juu ya mambo ambayo alifikiri kuwa ni mazito.

## SEHEMU B (Alama 20)

## UTUMIZI WA LUGHA NA USAHIHI WA MAANDISHI

3. Zitafakari kwa makini orodha A na B kisha eleza maana ya vifungu vya maneno katika orodha A kwa kutumia orodha B.

ORODHA A

(i) Ngeli
(ii) Sentensi sahili
(iii) Nomino za pekee
(iv) Neno lenye fonimu nne (4)
(v) Kiambishi cha nafsi ya pili (2) wingi

ORODHA B

A Pangani, Asha, usingizi na John
B Anayesinzia ni mvivu
C Chaki
D PAMUKA
E Wanaimba
F Mnaimba
G Ku-
H Chai
I Kariakoo, Tanga, Iringa na Ali
J Wewe ni mvivu



Find more free educational resources at http://maktaba.tetea.org

4. Sentensi zifuatazo zina makosa. Ziandike vizuri kwa kuepuka hayo makosa yaliyojitokeza.

(a) Nyinyi wote mna makosa.
(b) Mhasibu amewasilisha fedha mashuleni.
(c) Hupandaga mahindi shamba lote.
(d) Kinyonga kinabadili rangi.
(e) Mama alimpiga mwanae.

5. Taja mambo matano muhimu ya kuzingatia katika utungaji mzuri wa insha. Eleza umuhimu wa kila jambo.

## SEHEMU C (Alama 20)

## SARUFI

Jibu maswali yafuatayo kwa kutoa maelezo mafupi.

6. Isitilahi moja inaweza ikawa na majina mawili. Andika jina lingine kwa kila moja ya dhana zifuatazo:

(a) Sentensi huru
(b) Kitenzi kikuu
(c) Kirai nomino
(d) Kitamkwa cha msingi.

7. Andika nomino tano (5) za ngeli ya Li-| ya – na kwa kila moja tunga sentensi ya umoja na wingi.

8. Tunga sentensi kisha onesha kishazi huru na kishazi tegemezi.

9. Eleza dhima ya mofimu "na" iliyopigiwa mstari.

(a) Asha na John wataoa<u>na</u>
(b) Ana<u>na</u>ta sana mtoto huyu
(c) <u>Na</u>ni kati yenu anajua kusoma vizuri?
(d) <u>Na</u>omba mtege masikio yenu vizuri.

## SEHEMU D (Alama 10)

## HISTORIA YA LUGHA

10. (a) Andika lahaja tano za kiswahili.

(b) Kabla ya uhuru, Waarabu walitumia njia gani ambazo zilisababisha kukua na kuenea kwa Kiswahili Tanzania?

## SEHEMU E (Alama 40)

## FASIHI

Jibu maswali MAWILI (2) kutoka sehemu hii. Swali la 12 ni la **lazima**.

11. Kwa kutumia mchoro vichambue vipera vya fasihi simulizi.

12. Fasihi ni chuo chenye kufundisha malezi kwa kila mwanajamii husika. Thibitisha hoja hiyo kwa kutumia vitabu viwili vya ushairi vilivyoorodheshwa hapo chini.

13. Onesha na jadili shida zinazojadiliwa na riwaya mbili kati ya zilizoorodheshwa hapo chini.

14. Wahusika na hasa mhusika mkuu katika tamthiliya ndiye anayeifikishia jamii ujumbe uliokusudiwa. Tumia tamthiliya mbili kati ya zilizoorodheshwa hapo chini kutetea hoja hiyo.


Find more free educational resources at http://maktaba.tetea.org

## ORODHA YA VITABU VITAKAVYOTUMIKA

**USHAIRI**

| | | |
|---|---|---|
| DIWANI YA MLOKA | - | C. Mloka (B.P) |
| DIWANI YA USTADH | - | A. Andanenga (B.P) |
| MALENGA WAPYA | - | TAKILUKI – (DUP) |

**RIWAYA**

| | | | |
|---|---|---|---|
| HIBA YA WIVU | - | Z. Mwanga | (R.P) |
| KUSADIKIKA | - | S. Robert | (Nelson) |
| ZAWADI YA USHINDI | - | B. Mtobwa | (R.P) |

**TAMTHILIYA**

| | | | |
|---|---|---|---|
| HAWALA YA FEDHA | - | A. Lihamba | (TPH) |
| MFALME JUHA | - | F. Topan | (DUP) |
| NGOSWE – Penzi Kitovu cha Uzembe | - | S. Semzaba | (ESC) |



Find more free educational resources at http://maktaba.tetea.org